

Nambari ya Mtahiniwa

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

133

KISWAHILI

MUDA : SAA 2.00

JUMATATU 27 NOVEMBA, 2017 mchana

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Jawabu zote ziandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA USAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 12 zenye maandishi

SEHEMU A: (Alama 15)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

Soma habari hii kwa makini kisha jibu maswali yafuatayo:

Wakazi wengi wa wilaya ya Monduli ni wafugaji. Baadhi yao wanahama mara kwa mara na mifugo yao. Wanafanya hivyo wakitafuta maji na chakula cha mifugo yao.

Kabla ya uhuru watu wa wilaya ya Monduli walikuwa hawana afya. Walikuwa wakinywa maji machafu. Walikuwa wakiyapata kwenye madimbwi. Mengine waliyapata katika mifereji na mabwawa. Mifugo yao ilitumia maji hayo pia. Maji hayo yalikuwa na takataka nyingi. Tena yalikuwa na vijidudu vya magonjwa.

Watu hawakuwa wanatumia vyoo. Mazingira yao yalikuwa machafu. Hawakujua kujikinga na magonjwa yanayotokana na uchafu. Hawakuelewa mambo yaliyosababisha wapate minyoo. Walikuwa wakijikuna mara kwa mara. Magonjwa ya macho, vidonda na kuharisha yaliwasumbua kwa muda mrefu na hawakujua sababu. Watoto wao walikuwa na utapiamlo. Vile vile walisumbuliwa na surua, pepopunda na homa ya manjano. Wengi wao walidhoofu.

Baada ya uhuru Serikali yetu iliamua kusogeza huduma muhimu za kijamii vijijini. Ili kazi zifanikiwe, mikoa ilipaswa kuzisimamia. Serikali ilipanga kuwa kila kijiji kipate maji safi na salama ya kutosha. Kazi ya kutafuta maeneo yanayofaa kwa ajili ya kuchimba visima katika wilaya ya Monduli ilianza. Visima vilichimbwa na vyengine vinaendelea kuchimbwa. Visima hivyo vimeanza kupunguza tatizo la maji. Maeneo mengine kama Monduli mjini, Mto wa Mbu na Mererani kuna maji ya bomba. Maji ya bomba yanaendelea kuenezwa katika maeneo mengi. Maeneo yenye tatizo la maji si mengi tena kama ilivyokuwa kabla ya uhuru.

Serikali pia imejenga vituo vya afya na hospitali ya wilaya mjini Monduli. Vituo vya afya vinatoa elimu ya afya kwa watu wote. Watoto hupatiwa chanjo. Vifo vya watoto na magonjwa ya kuambukiza yamepunguwa.

Ili kupunguza msongamano wa watu katika vituo vya afya, Serikali pia imeruhusu ujenzi wa hospitali za watu binafsi na hospitali za Mashirika ya dini.

1. Maswali.

a) Kwa nini baadhi ya wakazi wa Monduli wanahama mara kwa mara?

b) Elezea kwa ufupi mambo yaliyokuwa yakiwasumbua watu wa Monduli.

c) Watu wa Monduli walikuwa wakipata wapi maji ya kunywa kabla ya uhuru?

d) Taja sababu mbili (2) zilizopelekea vifo vya watoto na magonjwa ya kuambukiza kupungua katika Wilaya ya Monduli.

e) Lete kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari.

2. Fupisha aya ya tatu ya habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi kumi na tano (15).

SEHEMU B: (Alama 40)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii. (Swali la sita (6) ni la lazima)

3. Tunga sentensi tano (5) zenye vivumishi vifuatavyo. (Pigia mstari vivumishi hivyo).

a) Kivumishi cha sifa.

b) Kivumishi cha idadi.

c) Kivumishi cha a-unganifu.

d) Kivumishi cha kuonesha.

e) Kivumishi kimilikishi.

4. Tunga sentensi zenye muundo ufuatao:-

a) N + T + E

b) N + V + T + N

c) W + T + E

d) H + N + T + N

e) W + V + T + N

5. Tafsiri sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

a) There are thirty five mangoes in the basket.

b) Our cat has three pretty kittens.

c) The rain of this year causes flood in many areas.

d) You are watering your garden very well.

e) When will you go to visit your sister in law?

Nambari ya Mtahiniwa

6. Oanisha tarakimu kutoka sehemu A na maneno sahihi kutoka sehemu B kwa kuweka herufi sahihi katika nafasi zilizo wazi.

Sehemu A			Sehemu B
i)	_____	160,000	A: Laki nne elfu sitini na tisa mia nane na tisini.
ii)	_____	387,074	B: Efu kumi na sita.
iii)	_____	469,890	C: Milioni moja laki sita.
iv)	_____	1,600,000	D: Laki moja na elfu sitini.
v)	_____	106,025	E: Laki moja elfu sita na ishirini na tano.
			F: Laki tatu elfu themanini na saba na sabini na nne.
			G: Milioni moja elfu sita na ishirini na tano.

7. Fupisha sentensi zifuatazo:

a) Asha alinunua mbatata, tungule, bilingani na embe mbichi.

b) Bibi anauza kata, chungio, chujio, mwiko, upawa na chuma cha mikate.

c) Skuli yetu tunalima mtama, maharage, mpunga, kunde na choroko.

d) Baba alileta embe, machungwa, nanasi , tikiti na ndizi.

Nambari ya Mtahiniwa

- e) Wageni walikaribishwa soda, juisi na togwa.

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) tu katika sehemu hii

8. Tunga beti nne (4) za utenzi unaohusu “Malezi ya Watoto”.

[illegible]

9. Elezea kwa ufupi mafunzo ya methali zifuatazo:

a) Mgagaa na upwa hali wali mkavu.

b) Mchamago hanyele huenda akawia papo.

c) Muangaza mbili moja humponya.

d) Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

e) Pili pili usiyoila inakuwashia nini?

10. Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Hospitali hakika,	utatibiwa lazima.
Hivyo usifanye shaka,	utarudia uzima.
Lakini kwanza kumbuka,	maneno niliyosema.
Hifadhi njema ya mwili,	ndiyo kinga ymaradhi.

Nambari ya Mtahiniwa

Shida ya ugonjwa wako, hukula chakula chema.
Na pengine kula kwako, wakati hukutizama.
Au uliwacha mwiko, usafi hukuupima.
Hifadhi njema ya mwili, ndio kinga ya maradhi.

Tumbo lapiga kelele, tena linanguruma.
Laonesha liko tele, choo hukupata vyema.
Sasa linaleta ndwele, mwenyewe unalalama.
Hifadhi njema ya mwili, ndiyo kinga ya maradhi.

Viungo mwavipa tabu, hebu oneni huruma.
Hwenda mukaviharibu, mukashindwa kuvituma.
Vikawatia adhabu, hatima vikawauma.
Hifadhi njema ya mwili, ndiyo kinga ya maradhi.

Maswali:

a) Shari hili lina beti ngapi?

b) Andika mshororo wa pili wa beti ya tatu.

c) Shairi hili lina mizani ngapi?

- d) Taja kina cha kati na cha mwisho katika ubeti wa kwanza wa shairi hili.

- e) Andika kibwagizo cha shairi hili.

SEHEMU D: (Alama 15)

UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii

11. Tunga Insha ya maneno yasiyopungua 120 kati ya moja ya mada zifuatazo:

- a) Umuhimu wa uhifadhi mazingira
b) Siku nisiyoisahau maishani mwangu

This image shows a single sheet of white paper with horizontal blue ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

- [illegible]

Nambari ya Mtahiniwa
